## FURSA YA KUWASILISHA MAOMBI

### UTARATIBU WA KUWASILISHA OMBI

Mfuko wa Vijana wa Haki na Usawa katika Mabadiliko ya Tabianchi (YCJF) unakusudia kutoa ufadhili wa kifedha kwa vikundi na taasisi za vijana zinazojihusisha na haki katika tabianchi. Vikundi vinakaribishwa kuwasilisha maombi ya ufadhili hadi USD 10,000, fedha ambayo inaweza kutumika kwa muda wa miezi 12.

### VIGEZO VYA KUKIDHI KUWASILISHA OMBI

Endapo utapenda kuwasilisha maombi, zingatia na ukidhi vigezo vilivyoorodheswa hapa chini. Mtandao, taasisi au kikundi chako lazima kiwe:

- kinaongozwa na vijana wenye umri wa miaka 35 na chini. Kustahili ruzuku ya YCJF, wanachama/ wajumbe wengi wa taasisi yako wanapaswa kuwa vijana walio na umri wa chini ya miaka 35, na hata uongozi au watu walio na nafasi za utawala wanahitaji kuwa vijana wenye umri wa miaka 35 na chini;
- kiko Afrika; Asia na Pasifiki; Amerika ya Kusini na Karibiani; na Ulaya ya Kati, na Mashariki;
- kiko Amerika Kaskazini au Ulaya Magharibi lakini uongozi wake ni vijana wanaobaguliwa na/au kutengwa kwa misingi ya tabaka, kabila, asili n.k;
- hakifungamani kisiasa na vyama, hakina vurugu, na kina usajili halali wa kisheria;
- kinaamini na kuonyesha kwa uthabiti jitihada shirikishi katika mipango na maandalizi, utekelezaji wa pamoja, na ubia mtambuka.

Tunatafuta haswa vikundi vinavyojihusisha na:

- Kukuza uongozi uliojikita katika misingi ya haki na usawa katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi, na haswa kwa nguvu ya jamii.
- Kukuza matarajio, utayari na ahadi kwenye haki na usawa wa tabianchi, jamii na mazingira.
- Kuwawajibisha watunga sera kwa ahadi zao na kuimarisha nguvu za jamii.

### MCHAKATO WETU

Ufadhili shirikishi wa Youth Climate Justice Fund.

1) Tangazo la wito na fursa ya kuwasilisha maombi

Fursa hii ya kuwasilisha maombi iko wazi kwa muda wa majuma manne (4), taasisi na mitandao ya vijana inayojihusishana Haki na Usawa katika Mabadiliko ya Tabianchi duniani, wanakaribishwa kuwasilisha maombi. Kwa mitandao, taasisi na vikundi visivyozungumza Kiingereza wanakaribishwa kuwasiliana na Viongozi wa Kanda kwa usaidizi wa kutuma maombi katika lugha yao wenyewe.

2) Maombi kupitiwa na kuchaguliwa na wafanyakazi wa YCJF

Wafanyakazi wa YJCF watahakikisha kuwa kikundi chako kimetimiza na kukidhi vigezo vya msingi, na kinawiana na thamani na kanuni za YCJF.

3) Maombi kupitiwa na Viongozi wa Kanda

Mawasilisho yatapitiwa kadiri ya vipaumbele vya kila kanda/ bara, na inapowezekana kuwasiliana na vikundi kuelewa zaidi mahitaji yao.

4) Maombi kupigiwa kura na Kamati ya Utendaji

Kila mjumbe wa kamati ya utendaji hutoa alama na kupanga vikundi kulingana na kanuni, viwango na vipaumbele vya ufadhili vya YCJF.

5) Taratibu za uhakiki taasisi

Wafanyakazi na Viongozi wa Kanda/ Bara watawasiliana na vikundi vilivyochaguliwa kupokea ufadhili, ili kuhakiki habari zao.

6) Kutoa ruzuku/ ufadhili wa kifedha

Wafanyakazi na Viongozi wa Kanda/ Bara watafanya kazi na wabia ili kufanikisha upatikanaji wa ruzuku/ fedha za ufadhili.

7) Kujiunga na jumuiya ya YCJF

Vikundi vinaalikwa kujiunga na wito wa kuwakaribisha wa YCJF na kushirikiana kukuza rasilimali za kukuza uwezo wa vijana hadi vijana.

**Maswali yanayoulizwa mara kwa mara**

Tuko dhahiri na tuna uthubuti thabiti katika kubadilika na kukua ili kuhakikisha mitandao ya vijana ya Haki na Usawa wa Mabadiliko ya Tabianchi wanawezeshwa kushikiriki na kupata usaidizi, kadri tunavyoendelea kuweka taratibu zetu, mifumo na mazingira rafiki kwa ajili ya kuboresha michakato yetu na ushirikishwaji bora.

Haya ni maswali 10 ambayo yanaweza kukusaidia katika maombi yako, ikiwa swali lako halijajibiwa, tutumie barua pepe kwa ask@ycjf.org

- **Je, tunamaanisha nini 'kushughulikia haki katika mabadiliko ya tabianchi na usawa wa kijamii na kimazingira'?**
    - Tunamaanisha shughuli, maamuzi, kampeni, na miradi inayoshughulikia matatizo ya mabadiliko ya tabianchi kwa kutatua changamoto za ubaguzi, unyonyaji na ukandamizaji, na kuimarisha usawa, haki na demokrasia katika jamii.

- **Tunamaanisha nini 'kuongozwa na vijana'?**
    - Tunaamini kwamba neno "vijana" lina maana nyingi na miktadha kutegemea mitazamo na miktadha ya ulimwengu. Tunaamini ni muhimu kuwahusisha vijana wakubwa chini ya umri wa miaka 35 ambao wanabaguliwa au kutengwa kwa misingi ya tabaka, kabila, utambulisho wa Watu wa Asili, jinsia, n.k. na wanaharakati wachanga sana ambao pia wanakabiliwa na vikwazo sawa vya kimfumo.

- **Je, mpango wa kuwezesha "vijana-kwa-vijana" ni nini?**
    - Vijana kushirikiana na kusaidia katika kukuza uwezo kupitia kuwezesha rika, ndio namna bora ya kutoa huduma za maendeleo kutokana na uzoefu na uelewa wa pamoja wa vijana. Tutashirikiana kujenga na kuboresha uwezeshaji rika wa vijana kwa vijana kulingana na kila kundi la washirika wanaopokea ruzuku.

- **Je, tunawezaje kuomba uwezeshaji na usaidizi usio wa kifedha?**

- Tafadhali wasiliana na kiongozi wetu wa Mkoa au tuma barua pepe kwa ask@ycjf.org

- **Je, nini ni vyanzo vyenu vya fedha za ufadhili?**
    - Gharama zetu za awali za usanidi na ufadhili inatolewa na watu binafsi na wahisani – kuliko kampuni binafsi. Hatupokei fedha kutoka kwa mtu yeyote ambaye haendani na kanuni, viwango na maadili yetu.

- **Je, maombi lazima yawe kwa Kiingereza?**
    - Iwapo unahitaji usaidizi wa kutuma maombi katika lugha nyingine, pakua kifurushi chetu cha maombi ambacho kinapatikana katika lugha 7 (Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kihindi, Kireno, Kihispania na Kiswahili). Zaidi ya hayo, unaweza kuwasiliana na ask@ycjf.org ili kuwasiliana na Kiongozi wa Kanda/ Bara ambaye anaweza kukusaidia kutuma ombi katika lugha unayopendelea.

- **Je, tunahitaji kusajiliwa kisheria?**
    - Hapana, sio lazima. Mara nyingi, vikundi visivyo rasmi vimekuwa na mchango kubwa kijamii na kimaendeleo bila usajili rasmi au kwa kukosa rasilimali muhimu za kujiandikisha. Tunatamani kugundua njia bunifu za kusaidia vikundi kama hivyo.

- **Hatuwezi kupata au kutumia fomu ya maombi ya mtandaoni, je tunaweza kupata usaidizi?**
    - Bila shaka, tuma barua pepe ask@ycjf.org na tutafanya tuwezavyo kukusaidia.

- **Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha pendekezo langu ni lini?**
    - Unaweza kutuma maombi yako kati ya tarehe 21 Agosti na 24 Septemba.

- **Je, tunaweza kuomba hadi $10.000 USD, lakini je, tunaweza kutuma ombi hata kama jumuiya yetu inahitaji ufadhili zaidi?**

- Tunafahamu kwamba vikundi vinaweza kuhitaji ufadhili zaidi ili kufikia matokeo fulani, ikiwa utahitaji usaidizi zaidi wa ufadhili, tafadhali tuma barua pepe kwa ask@ycjf.org

**JE, UKO TAYARI KUTUMA OMBI? HAYA NDIYO TUNAYOULIZA KATIKA FOMU YETU YA MAOMBI:**

**SEHEMU A - VIGEZO VYA KUKIDHI**

- Je, wewe ni taasisi inayoongozwa na vijana?
    - Ndio/ Hapana
- Taasisi yako yako iko kanda/ bara gani?
- Je, taasisi yako ina bajeti ya kila mwaka?
    - Ndio/ Hapana
- Kama Ndio, bajeti yako ya mwaka ni kiasi gani?
    - Bajeti katika USD
        - 0 - 10,000
        - 10-25,000
        - 25-50,000
        - 50,000 - 100,000
        - 100,000+

**SEHEMU B - MAELEZO YA KUNDI / MRADI**

1. Jina la Taasisi/Kikundi chako

    Jibu fupi

2. Anwani ya kudumu ya taasisi yako ?

    Jibu fupi

3. Jina la Kiongozi wa Mradi Pendekezwa

    Jibu fupi

4. Nafasi ya Kiongozi wa Mradi Pendekezwa katika taasisi

Jibu fupi

5. Tarehe ya kuzaliwa

    DD/MM/YYYY

6. Mawasiliano (barua pepe/ WhatsApp/ Telegram/ Signal / Simu ya mezani/ kiganjani)

    Jibu fupi

7. Je, nini ni dira ya kimkakati na lengo kuu la taasisi yako?

    Jibu fupi

8. Je, unaomba kiasi gani cha ufadhili kifedha?

    Jibu fupi

9. Utatumia fedha ya ufadhili katika shughuli gani?

    Jibu fupi - tafadhali ambatanisha bajeti yako na mchanganuo katika swali la mwisho (maneno yasiyozidi 100)

10. Je, una mahitaji gani ya uwezeshwaji kando ya ufadhili wa kifedha?

    Jibu fupi (Tunawezaje kukusaidia zaidi ya ruzuku hii)

11. Eleza kwa ufupi mradi/shughuli kuu unayotafuta ufadhili kwayo

    Jibu fupi (maneno yasizidi 200 - hii inaweza kuwa kitu chochote kutoka kwa shughuli maalum za shirika lako au kutunza tu wafanyikazi wako na gharama za uendeshaji)

12. Je, nini ni mafanikio ya taasisi yakp hata sasa, na ni kwa namna gani fedha kutoka mfuko huu utaboresha zaidi na kuendeleza juu ya mafanikio ya awali?

    Jibu fupi (eleza kwa ufupi tatizo ulilotambua na kushughulikia hapo awali, na jinsi uzoefu huo unavyoweza kuongezwa kwa ruzuku hii)

13. Orodhesha washirika au wabia wowote unaofanya /ungependa kufanya kazi nao kwenye mpango huu.

    Jibu fupi (maneno yasizidi 100)

14. Ni kwa namna gani taasisi yako inazingatia/ inapanga kuzingatia kanuni za haki, usawa, umoja katika utofauti na ushikirishwaji katika jitihada na shughuli za kusaidia makundi yasiyo kipaumbele au yasiyojiweza?

    Jibu fupi (maneno yasizidi 100)

15. Unaiona wapi taasisi yako miaka 3 kutoka sasa?

    Jibu fupi (maneno yasizidi 100)

16. Tafadhali wasilisha nyaraka, tovuti, au faili linalowakilisha kazi au ombi lako (ikiwezekana: bajeti na mchanganuo, ni lazima na unaweza kuongeza taarifa za shughuli zako za hivi karibuni , au kitu chochote unachoona kinafaa )?

Je, uko tayari kutuma maombi? Tembelea tovuti hii kuwasilisha.
Ikiwa unahitaji usaidizi wowote wa kukamilisha ombi lako kwa sababu ya vikwazo vya lugha au teknolojia, au ukosefu wa ufafanuzi, tafadhali wasiliana na Viongozi wetu wa Kanda/ Bara kupitia [ask@ycjf.org](mailto:ask@ycjf.org)